

**UCHANGANUZI WA MAKOSA YA MSAMIATI WA KISWAHILI KATIKA MATINI
ANDISHI ZA HABARI: MFANO WA *BBC SWAHILI* NA *DW KISWAHILI***

Alcheraus R. Mushumbwa

Ikisiri

*Makala hii imechunguza makosa ya msamiati yanayofanyika katika vyombo vya habari vya *BBC Swahili* na *DW Kiswahili*. Istilahi msamiati, katika makala hii, inatumika kwa maana ya maneno yote yanayotumika katika lugha (TATAKI, 2013:384 na BAKITA, 2015:701). Malengo ya makala ilikuwa ni kuchanganua makosa ya msamiati, kubainisha sababu za makosa ya msamiati na athari za makosa hayo katika lugha. Ili kutimiza madhumuni ya Makala hii, kiunzi cha uchanganuzi wa habari kiisimu (van Dijk, 1988) kilizingatiwa. Sampuli ya utafiti huu ilihusisha matini ishirini za habari zilizosomwa kutoka kwenye tovuti za vyombo vya habari vilivyochunguzwa. Matokeo ya uchunguzi wa makala inaonesha kuwa vyombo vya habari vya *BBC* na *DW* (Idhaa za *Kiswahili*) hufanya makosa yanayohusu msamiati wa *Kiswahili* katika kuripoti habari kwa maandishi. Makosa hayo ni uunganishaji na utenganishaji wa maneno, uchopekaji na udondoshaji wa vipashio vinavyounda maneno, matumizi ya neno lisilofaa na utohozi wa maneno. Vilevile, makala ilibaini kwamba makosa hayo yalisababishwa na umilisi hafifu wa msamiati wa *Kiswahili*; athari ya lugha ya mazungumzo na lugha za kigeni. Mwisho, makala ilibaini kuwa makosa hayo yana athari kwa watumiaji wa *Kiswahili* na kupendekeza namna ya kuyaepuka.*

Utangulizi

Shoo (2004) anadai kwamba pamoja na vyombo vya habari kuwa na mchango mkubwa katika ukuzaji na uenezaji wa *Kiswahili*; vilevile, vyombo hivyo huchangia kwa namna fulani kufanya makosa mbalimbali yanayorudisha nyuma ustawi wa *Kiswahili*. Shoo (keshatajwa) anataja *BBC Swahili* na *DW Kiswahili* kama vyombo vyenye kusheheni matumizi mabaya ya maneno. Kutokana na madai hayo, mtafiti aliamua kufanya utafiti zaidi ili kujua aina za makosa yanayohusu msamiati katika matini za habari za vyombo hivi viwili, yaani *BBC* na *DW*. Hata hivyo, Shoo (keshatajwa) hakunua kuchunguza makosa katika vyombo vya habari bali alichambua umuhimu na nafasi ya *Kiswahili* katika vyombo vya habari. Hivyo, alitaja makosa kama sehemu ya kikwazo cha kustawisha *Kiswahili* katika karne ya 21 kwenye vyombo hivyo.

Madhumuni ya makala hii ni kuchunguza makosa yanayohusu msamiati kwenye matini andishi za habari. Kwa kuwa maneno ni nguzo muhimu ya lugha (Kordjazi, 2011; Tanyer & Ozturk, 2014; Alqahtani, 2015 na Viera, 2017), matumizi sahihi na bora ya msamiati katika kuwasiliana ni jambo muhimu sana. Katika uandishi wowote, maneno au msamiati ni kiungo muhimu katika kufanikisha zoezi la utoaji wa taarifa iliyokusudiwa. Hata hivyo, matumizi ya msamiati yanahitaji umakini kwa sababu waandishi wengi hufanya makosa yanayohusu msamiati kwa namna mbalimbali (Jurianto, 2015). Hivyo basi, ili kuepuka tatizo hili yafaa kwa mwandishi kuwa makini wakati wa kuandika maneno. Sawa na watumiaji wengine wa lugha, waandishi wa habari nao hufanya makosa yanayohusu msamiati katika habari wanazoandika. Hivyo basi, malengo ya uchunguzi wa makala hii ni: (a) Kuchanganua makosa ya msamiati wa Kiswahili katika matini andishi za habari; (b) Kubainisha sababu za makosa ya msamiati wa Kiswahili katika matini andishi za habari; na (c) Kufafanua athari za makosa ya msamiati wa Kiswahili yaliyopatikana katika matini za habari.

Mapitio ya Maandiko

Telg (2015) anaeleza kuwa mwandishi wa habari anapaswa kuandika na kutamka maneno kwa usahihi na jinsi inavyotakiwa. Anaendelea kusesitiza kuwa inampasa mwandishi wa habari kuepuka makosa kama ya tahajia, vifupisho visivyotambulika na kutumia ishara. Aidha, Hasani (2004) anabaini kuwapo kwa makosa ya kiisimu ya kiutamkaji, kisemantiki na kisarufi katika shirika la habari la Iran (katika Akbari & Kheirabadi, 2015). Akbari & Kheirabadi (keshatajwa), wanaonesha kuwa makosa ya kimsamiati, urudiaji wa maneno, ukosefu wa ushikamani, tahajia na uchapaji wa maneno yalibainika kwenye habari za vyombo vya Irani. Kwa upande mwingine, Zafar (2016) anabainisha kwamba matangazo ya vyakula katika magazeti nchini Pakistani hutumia vyema msamiati na istilahi katika kutangaza bidhaa hizo. Gbara (2001) alichunguza makosa ya kisarufi katika magazeti na athari zake kwa hadhira nchini Nigeria. Utafiti huo ulibaini kuwa waandishi wa habari walifanya makosa ya msamiati kama vile matumizi ya maneno yasiyo sahihi, unyambulishaji wa maneno usiotakiwa na matumizi mabaya ya vibainishi.

Kwa upande wa vyombo vya habari vya Kiswahili, makosa mbalimbali ya msamiati hufanywa. Kihore (2004) anaonesha kuwa magazeti ya Kiswahili ya mitaani nchini Tanzania, husheheni matumizi mengi ya maneno ya mkopo kutoka lugha ya Kiingereza; hufuata miundo ya lugha ya Kiingereza na hutumia msamiati ambao si sanifu. King’ei (2000) anathibitisha kwamba kwenye vyombo vya habari vya Kenya, kuna hali ya kutomudu msamiati vizuri. King’ei (keshatajwa) anashadidia hoja yake kwa kueleza kwamba makosa ya matamshi, wingi na uchache, tafsiri na utohazi hudhihirika kwenye vyombo hivyo. Onyango & Odawo (2016) wanaeleza kuwa kuna makosa mengi ya msamiati wa Kiswahili yanayofanywa na wanahabari. Wanataja baadhi ya makosa hayo wakimnukuu Mbaabu (1991) kuwa ni uvurugaji wa ngeli kiholela na matumizi ya tafsiri sisizi (Onyango & Odawo, keshatajwa). Kwa mujibu wa Shoo (keshatajwa), vyombo vya habari vinavyotumia Kiswahili hasa magazeti na redio, hutumia baadhi ya maneno ya Kiswahili kimakosa, ikiwamo *BBC* na *DW*. Shoo (keshatajwa) anataja mifano ya maneno yanayotumika vibaya kwenye vyombo vya habari kama vile *denti*, *teja*, *uroda*, *noma*, *aidha*, *vinjari* na *mhanga*. Simba (1995) anakiri kuwa katika vyombo vya habari vya Kiswahili yapo makosa kadhaa yakiwamo yale ya msamiati kama kutotamka na kutoandika maneno kwa usahihi na kutumia maneno yasiyo sanifu.

Kulingana na wataalamu mbalimbali, makosa ya lugha hufanyika kwenye vyombo vya habari. Hata hiyo, wataalamu tuliowapitia hawakushughulikia kwa kina makosa ya msamiati wa Kiswahili katika vyombo vya habari vya *BBC* na *DW*. Kutokana na pengo hilo la kimaarifa, makala hii imebainisha na kuchanganua makosa ya msamiati wa Kiswahili kwa upekee, mifano ikitolewa kutoka kwenye habari andishi za *BBC Swahili* na *DW Kiswahili*.

Mkabala wa kinadharia

Utafiti huu umeongozwa na *kiunzi cha uchanganuzi wa habari kiisimu*. Kiunzi hiki ni miongoni mwa viunzi vinavyounda nadharia ya *uchanganuzi wa habari kama matini/usemi (news as discourse)* iliyoasisiwa na Teun A. van Dijk (1988). Kwa mujibu wa van Dijk (keshatajwa), habari inapochanganuliwa kiisimu ni sharti mchanganuzi azingatie kanuni zinazoongoza kila kipengele cha lugha husika. Hoja ya msingi ya van Dijk (keshatajwa) ni kwamba kanuni

zinazoongoza matumizi ya lugha kwa kila kipengele zinapaswa kuzingatiwa katika kuchanganua matini za habari kwa mtazamo wa kiisimu. Hii ni kusema kuwa matumizi ya lugha katika vyombo vya habari yanapaswa kuzingatia ufasaha na usanifu wa lugha ambao unaongozwa na sheria za kila kipengele. Vipengele vya lugha anavyosisitiza van Dijk (keshatajwa) ni pamoja na msamiati, matamshi, miundo, maana, mantiki na maumbo. Kulingana na van Dijk (keshatajwa), matumizi ya lugha katika vyombo vya habari hasa vyombo rasmi, yanapaswa kuwa ni sanifu na fasaaha, yanayofuata uteuzi wa maneno sanifu, miundo changamano, sentensi zinazoeleweka na zenye mantiki inayoletwa na vishikamanishi. Kanuni za ushikamani na uteuzi wa msamiati sahihi hufanya habari iwe matini iliyojengwa kwa miandamo inayokamilisha kitu kizima chenye maana kamili.

Katika makala hii, tumechunguza matumizi sahihi ya msamiati wa Kiswahili kwenye matini za habari na kubaini makosa yaliyofanyika kuhusu msamiati huo. Matumizi ya msamiati wa Kiswahili hupaswa kuzingatia usanifu na ufasaha, uandishi sahihi na uteuzi wa msamiati unaofaa. Ukiukwaji wa kanuni hizo, husababisha makosa ya msamiati ambayo huweza kuharibu ufasaha wa lugha katika habari.

Mbinu za utafiti

Utafiti wa makala hii umetumia mkabala wa kitaamuli katika kuchanganua na kujadili data. Data zilikusanywa kutoka kwenye vyombo vya habari vya *BBC Swahili* na *DW Kiswahili*. Matini za habari zilizosomwa zilipatikana kwenye tovuti za vyombo hivyo ambazo ni: <https://www.bbc.com/swahili> na <https://www.dw.com/sw/idhaa-ya-kiswahili> kati ya mwezi Februari na Juni, 2019. Mwandishi wa makala hii alisoma kwa makini matini 20 za habari zilizochapishwa kwenye tovuti hizo. Usomaji ulizingatia habari zilizoarifu matukio mbalimbali. Kila mwezi, mtafiti alipanga kusoma matini 4 za habari zilizochapishwa ndani ya saa 48 tangu kuripotiwa kwazo. Mwandishi alinukuu makosa ya msamiati yaliyojitokeza kwa kila makala iliyosomwa. Mara baada ya kubaini makosa, yaliainishwa kimakundi, yakafafanuliwa moja baada ya jingine na kuyasahihisha. Pia, mwandishi alifafanua vyanzo na athari za makosa yaliyochunguzwa.

Makosa ya msamiati katika matini za *BBC Swahili* na *DW Kiswahili*

Kabla ya kuanza uchanganuzi wa data, ni vizuri kueleza maana ya makosa kama yanavyochukuliwa kwenye makala hi. Kwa kuzingatia fasili ya TATAKI (keshatajwa), kosa *ni kufanya lisilo sahihi au lisilokubalika*. Fasili hii ndiyo inayochukuliwa katika makala hii. Hivyo, makosa ya msamiati ni *matamshi au maandishi yanayokiuka matumizi sahihi (kwenye maandishi au mazungumzo) ya maneno ya Kiswahili katika mawasiliano*. Uchunguzi wa makala hii ulibainisha makosa mbalimbali ya msamiati katika matini za habari zilizotafitiwa. Makosa hayo ni: uunganishaji wa maneno, matumizi ya neno lisilofaa, udondoshaji na uchopekaji wa vipashio vinavyounda maneno, na utohozi usiostahili.

Kosa la uunganishaji wa maneno

Kwenye Kiswahili, si kila neno hufaa kuunganishwa na jingine kuwa neno moja. Mathalani, kuandika *kwamfano* (badala ya “kwa mfano”) na *badalayake* (badala ya “badala yake”) ni makosa. Makala hii imebaini kuwa kulikuwa na maneno yaliyounganishwa kimakosa kwenye habari zilizochunguzwa. Jedwali lifuatalo linaonesha mifano ya makosa hayo.

Jedwali la 1. Makosa ya uunganishaji wa maneno

Na.	Kosa	Sahihi
a.	<i>Hatahivyo ...</i>	Hata hivyo...
b.	<i>Kwanini...</i>	Kwa nini...
c.	<i>Kwamujibuwa taarifa...</i>	Kwa mujibu wa taarifa...
d.	<i>Hivyobasi ndio maana nikasema</i>	Hivyo basi ndio maana nikasema...
e.	<i>Kwasababuhujui dhamira yao...</i>	Kwa sababu hujui dhamira yao...
f.	<i>...kwa kuwapajukumu hilo...</i>	...kwa kuwapa jukumu hilo...
g.	<i>Ziara yake nchini Tanzania inalengo...</i>	Ziara yake nchini Tanzania ina lengo
h.	<i>Kwasasa ...</i>	Kwa sasa ...
i.	<i>Ensemble inaviti 163 bungeni...</i>	Ensemble ina viti 163 bungeni...

j.	Moise Katumbi <i>ananafasi kubwa...</i>	Moise Katumbi ana nafasi kubwa...
----	---	-----------------------------------

Data hii inaonesha kosa la kuunganisha maneno ya Kiswahili ambayo hayapaswi kuunganishwa kama neno moja. Upo utaratibu wa kuunganisha maneno katika Kiswahili ili kuunda neno au istilahi mpya. Hata hivyo, kanuni hii haitumiki kwa kila neno. Kwa mujibu wa data ya hapo juu, uunganishaji wa maneno visivyo ulihusu maneno yaliyohusisha kiunganishi ‘kwa’ na vielezi ‘sasa, mujibu’, nomino ‘sababu’, kiwakilishi ‘nini’. Vilevile, tungo zilizojenga viunganishi vya mwendelezo kama ‘hata hivyo, hivyo basi’ zilidhihirisha kosa la kuunganishwa kwa maneno. Kosa jingine lilifanyika kati ya kitenzi na nomino kama ‘ana nafasi’, ‘ina vita’, ‘ina lengo’, ‘kuwapa jukumu’. Kutokana na ushahidi huu, ni wazi kwamba lugha ya Kiswahili haikubali muunganisho wa maneno wa namna hiyo; kufanya hivyo ni kosa kimsamiati. Kwa mujibu wa Aruba (2017), maneno yanapotumiwa katika sentensi hutarajiwa yawasilishe ujumbe muhimu lakini yanapounganishwa na kuandikwa kama neno moja huwatatiza wasomaji. Maana inayokusudiwa inaweza kupotea na msomaji kupata maana isiyokusudiwa. Mipaka kati ya neno na neno inapaswa kuwa wazi ili pasiwe na utata wakati wa kusoma maandishi.

Kosa la kutumia neno lisilofaa

Ili mawasiliano yaweze kueleweka vizuri mtumiaji wa lugha anapaswa kutumia maneno yanayofaa kulingana na muktadha na ujumbe unaolengwa kuwasilishwa. Kwa mujibu wa Kemunto & Ontieri (2018), uteuzi wa msamiati usiofaa katika maandishi husababishwa na mtu kuwa na msamiati sahihi ila anashindwa kutofautisha msamiati gani mwafaka wa kutumia katika sentensi husika. Ifuatayo katika jedwali la 2 ni mifano ya kosa la kutumia neno lisilofaa.

Jedwali la 2. Makosa ya kutumia neno lisilofaa

Na.	Kosa	Sahihi
a.	<i>Viongozi wa maandamano wametoa wito wa kusalia majumbani...</i>	Viongozi wa maandamano wametoa wito wa kubaki nyumbani...
b.	<i>Safari ya wanawake watupu kwenda angani...</i>	Safari ya wanawake pekee kwenda angani...
c.	<i>...anataka asitishе kazi huko Las Palmas.</i>	...anataka astaafu akiwa huko Las Palmas.
d.	<i>Wakati siku mia moja zikitimu...</i>	Wakati siku mia moja zikitimia...

e.	<i>Aliyekuja katika nafasi ya pili, Jeremy Hunt ambaye ni waziri wa sasa wa mambo ya nje, ameambulia kura 43...</i>	Aliyepata nafasi ya pili/alijekuwa wa pili, Jeremy Hunt ambaye ni waziri wa sasa wa mambo ya nje, ameambulia kura 43...
f.	<i>Jana, bunge hilo la mjini London liliuangusha mswada uliowasilishwa...</i>	Jana, bunge hilo la mjini London liliukataa/liliupinga mswada uliowasilishwa...

Maneno yaliyopigiwa mstari hayakufaa kutumika kulingana na muktadha na maana iliyodhamiriwa. Neno *kusalia* humaanisha mabaki au kufanya tendo la kusali katika sehemu fulani, ila maana iliyokusudiwa na mwandishi katika habari hiyo ni *kubaki katika eneo fulani* kwani, habari hiyo ilielezea kuhusu wito uliotolewa na viongozi waliotaka raia wasishiriki maandamano wakibaki makwao. Kimantiki, kutumia neno *kusalia* katika muktadha ulioelezwa kwenye habari ni kosa. Vilevile, mwandishi wa habari alilenga kueleza utimilifu wa idadi ya siku ila ametumia neno *kutimu* ambalo, katika Kiswahili sanifu, hakuna kitenzi cha namna hiyo isipokuwa kuna *kutimia*. Kadhalika, neno *watupu* lenye maana ya bila kuwa na kitu ndani au utupu lilitumiwa visivyo kueleza kuwa waliohusika ni watu wa jinsia ya kike tu. Hivyo, neno lililopaswa kutumiwa ni *pekee*. Vivyo hivyo, kosa lilifanyika katika kutumia maneno *kuja* na *angusha* badala ya *shika/pata* na *kataa/pinga* kutokana na muktadha na maudhui ya habari husika. Kosa la kutumia msamiati usiofaa linabainishwa na King’ei (keshatajwa) anayetoa kauli kwamba maneno kama *kuangaliwa*, *astahiki*, *uchu*, *upepo* badala ya *kuchunguzwa*, *stadi/mahiri*, *tamaa*, *hewa* yalitumika katika vyombo vya habari kutokana na kiwango duni cha ujuzi wa msamiati miongoni mwa waandishi.

Kosa la udondoshaji na uchopekaji wa vipashio vya maneno

Kwa mujibu wa Ontieri (2015:6), udondoshaji ni kuondoa kipashio katika neno kwa njia inayokiuka taratibu za lugha. Matini zilizochunguzwa zilisheheni hali ya udondoshaji katika maneno. Kwa upande wa uchopekaji, Ontieri (keshatajwa) anafafanua kwamba ni hali ya kuongeza kipashio katika neno. Ontieri (keshatajwa) anaendelea kufafanua kwamba hali hiyo husababisha kuzalisha neno lililosheheni sauti ya ziada ambayo haikuwapo katika neno la msingi. Katika uchunguzi huu, neno moja lilikuwa na kipashio kilichochopekwa kimakosa.

Ikumbukwe kwamba, udondoshaji na uchopekaji ni kosa ikiwa kipashio kilichoongezwa au kuondolewa kwenye neno hakikustahili kuongezwa au kuondolewa. Mifano ifuatayo katika jedwali la 3 inaonesha makosa hayo.

Jedwali la 3. Makosa ya udondoshaji na uchopekaji wa vipashio vya maneno

Na.	Kosa	Sahihi
a.	<i>M<u>a</u>slahi</i>	Masilahi
b.	<i>H<u>a</u>tma</i>	Hatima
c.	<i>K<u>u</u>ako</i>	Kuwako
d.	<i>M<u>s</u>wa<u>q</u>da</i>	Mswada

Katika mfano wa kwanza hadi wa tatu, sauti zilizotakiwa kuwa sehemu ya maumbo ya maneno zilidondoshwa kinyume na usanifu wa maneno hayo. Sauti hizo ni /i/ na /w/ ambazo zilipaswa kuwa kwenye maneno *masilahi*, *hatima* na *kuwako*. Makosa haya yamekuwa ya kawaida mno na yamezoeleka kwa wazungumzaji wa Kiswahili kiasi cha kukumbwa na athari hizo katika maandishi. Kwa upande wa mfano wa nne, kosa ni la kuchopeka sauti /a/ ambayo haikustahili kuwapo.

Kosa la kutohoa maneno visivyo

Kutohoa ni kufanya au kubadilisha matamshi au maandishi/tahajia ya neno la lugha ya kigeni yalingane na matamshi au maandishi ya lugha nyingine au lugha ya kienyeji (TATAKI, keshatajwa na BAKITA, keshatajwa). Kila lugha huwa na utaratibu wake maalumu wa utohoaji wa maneno kama inavyoamuliwa na mamlaka inayosimamia lugha. Katika Kiswahili, utohoaji ni mbinu ya kuzalisha maneno mapya kutoka lugha nyingine. Hata hivyo, si kila utohoaji hukubalika katika Kiswahili. Hivyo, ni muhimu kuzingatia matamshi sahihi yanayokubalika katika Kiswahili wakati tunapotohoa maneno. Kwa mfano, maneno kama *soka*, *sketi*, *shule* yametoholewa na yanatumika katika Kiswahili kutoka kwenye maneno *soccer*, *skirt*, *schule*. Utohoaji unakuwa ni kosa la msamiati pale mtumiaji wa lugha anapobuni matamshi yake bila kuzingatia taratibu husika. Pia, utohoaji huwa ni kosa kama neno la kigeni tayari lina kisawe

chake katika Kiswahili lakini mtumiaji anateua kisawe kisichokubalika kwa matakwa yake. Makala hii ilibaini kosa la utohoaji kama ifuatavyo:

Jedwali la 4. Makosa ya kutohoa maneno visivyo

Na.	Kosa	Sahihi
a.	<u>Demokrasi</u> ...	Demokrasia...
b.	... <u>zita</u> kazolipeleka taifa hilo katika <u>demokrasi</u>zitakazolipeleka taifa hilo katika demokrasia...
c.	... <u>difenda</u> wa Arsenal Laurent Koscienly	...mlinzi/beki wa Arsenal Laurent Koscienly
d.	<u>Amesema ajenti</u> wake.	Amesema wakala wake.

Katika mfano wa kwanza na wa pili, matamshi na tahajia sahihi inayokubalika katika Kiswahili ni *demokrasia* na si *demokrasi*. Pia, katika mfano wa tatu neno la Kiingereza limetumika kwenye Kiswahili kama linavyoandikwa na kutamkwa kwenye Kiingereza ilihali neno hilo lina kisawe katika Kiswahili. Katika mpira wa miguu, neno *difenda* hurejelea mchezaji anayecheza nafasi ya nyuma baada ya mlinda mlango, na kwa Kiswahili sanifu ni *mlinzi/beki* lakini mwandishi aliandika *difenda*. Vivyo hivyo, katika mfano wa nne, neno lililotumiwa halikupaswa kwani *ajenti* (agent) lina kisawe sanifu katika Kiswahili ambacho ni *wakala*. Hivyo, hili ni kosa la utohoaji kwa sababu maneno yaliyotumika ni ya kigeni na yalikiuka kanuni za utohoaji katika Kiswahili. Kwa mujibu wa Jurianto (keshatajwa) na Aruba (keshatajwa), waandishi hufanya kosa la utohoaji wa maneno kwa sababu ya kutumia maneno ya mkopo.

Sababu za makosa ya msamiati katika matini za habari

Baada ya kujadili makosa ya msamiati, uchambuzi unaofuata unahusu sababu za kufanyika kwa makosa hayo kama ifuatavyo:

Umilisi hafifu wa msamiati wa Kiswahili

Umilisi ni maarifa na ujuzi anaokuwa nao mtu katika taaluma fulani (BAKITA, keshatajwa). Katika upande wa lugha, umilisi ni maarifa na uwezo wa mtu wa kutumia lugha (kuzungumza/kuandika na kuelewa) kwa ufasaha kutokana na kufahamu kanuni za lugha hiyo

(BAKITA, keshatajwa). Mtu asipokuwa na umilisi wa kutosha wa msamiati wa lugha atafanya makosa kadhaa ya msamiati katika mazungumzo au maandishi. Jambo hili lilisababisha makosa ya msamiati yaliyochanganuliwa katika makala hii. Sababu hii inathibitika katika makosa ya kuunganisha maneno na matumizi ya neno lisilofaa. Kwa mfano, kutojua kuwa ‘*kwa nini, kwa sababu* na *kwa sasa*’ ni maneno mawili yanayopaswa kutengwa katika maandishi, kulisababisha maandishi kuyaandika jinsi wanavyoyatamka kama ‘*kwanini, kwasababu* na *kwasasa*.’ Katika Kiswahili, *kwa* ni neno kamili ambalo ni kihusishi/kiunganishi na huandikwa kwa kutenganishwa na maneno yanayoambatana nalo katika tungo. Pia, maneno *nini, sababu, sasa* ni maneno yanayojitegemea, hayapaswi kuunganishwa na kihusishi/kiunganishi yakawa neno moja. Wa aidha, kutojua maana na matumizi sahihi ya maneno kulisababisha kutumia msamiati usiofaa. Maneno ‘*kusalia majumbani, wanawake watupu kwenda angani, na aliyekuja katika nafasi ya pili kwenye uchaguzi*’ yalitumiwa visivyo badala ya ‘*kubaki, pekee na aliyeshika/aliyefuatia*’ kulingana na muktadha wa matumizi yake katika habari yalimotumika.

Athari ya lugha ya mazungumzo katika maandishi

Kuna tofauti baina ya lugha ya mazungumzo na lugha ya maandishi. Baadhi ya taratibu hupatikana katika maandishi ila hazipatikani katika mazungumzo; mfano, matumizi ya alama za uandishi na nafasi za kutenga maneno katika tungo. Kadhalika, kuna baadhi ya taratibu zinapatikana katika mazungumzo lakini si kwenye maandishi. Baadhi ya maneno yanavyotamkwa ni tofauti na yanavyoandikwa. Kwa mfano, *mbeya* hutamkwa [mbea], *muhimu/mwalimu* hutamkwa [muhim/mwalim]. Katika kutamka maneno *mwalimu* na *muhimu*, sauti /u/ hudondoshwa lakini katika maandishi haidondoshwi. Kwa mantiki hii, inaonekana wazi kwamba kuna tofauti kati ya mazungumzo na maandishi. Kwenye utafiti huu, ilibainika kwamba lugha ya mazungumzo iliathiri maandishi ya matini zilizochunguzwa kwa kiasi fulani. Hii imeonekana katika kosa la uunganishaji wa maneno. Katika mazungumzo, tunazungumza bila kuonesha nafasi za kutenganisha maneno, hivyo mtu asiyemudu vizuri stadi ya kuandika atayaandika baadhi ya maneno kama yanavyotamkwa pale yanapokuwa yameambatana kama ‘*inalengo, kwamujibu, hivyobasi, inaviti, ananafasi*’ badala ya ‘*ina lengo, kwa mujibu, hivyo*

basi, ina viti, ana nafasi.’ Vilevile, athari ya lugha ya mazungumzo imesababisha kosa la udondoshaji katika maandishi. Maneno kama ‘*masilahi, kuwako, hatima*’ yaliandikwa kama *maslahi/maslai, kuako* na *hatma*.

Athari ya lugha za kigeni

Mtu anapojua lugha mbili au zaidi na kuzimudu zote kwa kiwango fulani, kwa vyovyote vile lugha moja itaathiri nyingine wakati wa matumizi ya lugha mojawapo miongoni mwa lugha anazozungumza. Hali hii huathiri hata lugha ya maandishi. Katika makala hii, athari za Kiingereza na Kiarabu zimethibitika. Athari ya Kiingereza ilitibitika katika kosa la utohoaji wa maneno ambapo maneno ya Kiingereza yaliandikwa kama yalivyo kwenye Kiingereza kwa hati za Kiswahili ila kwa matamshi ya Kiingereza. Maneno *demokrasia, wakala* na *mlinzi/beki* yaliandikwa kama ‘*demokrasi, ajenti* na *difenda.*’ Athari ya Kiarabu imeonekana kwenye kosa la uchopekaji wa irabu /a/ isiyotakiwa katika neno *mswaada* badala ya *mswada* na kudondoshwa kwa sauti /i/ katika maneno *maslahi* na *hatma* badala ya *masilahi* na *hatima*. Katika kutamka maneno *hatma* na *maslahi* kwenye lugha ya Kiarabu, sauti /i/ haipo ila kwa sababu maneno hayo yametoholewa na kutumika kwenye Kiswahili yamepewa sauti hiyo ili yaweze kuendana na utaratibu wa Kiswahili. Kwa hiyo, bila kuzingatia hilo waandishi waliandika kama walivyozoea kuyatamka kwenye lugha ya Kiarabu.

Athari za makosa ya msamiati

Makosa ya kiuandishi yanayofanywa katika vyombo vya habari huathiri hadhira ya habari hizo kwa njia tofauti. Massamba (1995) anasisitiza kwamba “hakuna mwalimu ambaye ufundishaji wake unaathiri wanafunzi kwa haraka, hukubalika kwa haraka na yale anayosema yakachukuliwa kuwa ndiyo thabiti kuzidi vyombo vya habari.” Maoni ya Massamba ni dhahiri yanaonesha nguvu ya vyombo vya habari katika kuiathiri hadhira. *BBC Swahili* na *DW Kiswahili* ni vyombo vya habari vikongwe vinavyorusha matangazo kwa Kiswahili kwa hadhira wanaojua Kiswahili. Kutokana na ukongwe huo, vyombo hivi vina hadhira kutoka maeneo mbalimbali ya dunia. Kwa hiyo, athari zake ni kubwa kwa hadhira na lugha yenyewe (Kiswahili).

Kwa upande wa hadhira, makosa ya msamiati katika habari za vyombo hivi huchukuliwa ni sahihi. Hali hii huwakumba wasikilizaji ambao hawana ujuzi wa kutosha wa kutambua makosa hayo kwa sababu wanaamini kuwa vyombo hivyo vina waandishi na watangazaji mashuhuri; hivyo, maneno wanayotumia huwa yako sahihi. Shoo (keshatajwa) akieleza hoja hii anasema kwamba:

Nguvu ya vyombo vya habari ni kubwa. Ndiyo sababu baada ya Redio Sauti ya Ujerumani na BBC kulitumia neno “muhanga” kwa nguvu zote kumaanisha watu au mtu aliyeathirika katika janga fulani, pamoja na kwamba si sahihi limejipenyeza na kudakwa na waandishi wa Tanzania na Kenya na linaendelea sasa kutaka kubadilishwa maana, na limebadilishwa maana hasa!

Tunaona kuwa makosa ya msamiati yanaenea na kutumiwa na hadhira ya vyombo vya habari kama alivyoeleza Shoo (keshatajwa). Vilevile, Massamba (keshatajwa) akijadili hoja hii anasema kuwa mara nyingi msikilizaji wa redio, mtazamaji wa televisheni au msomaji wa gazeti huchukulia kuwa kila kilichoandikwa au kusemwa katika vyombo hivyo ni sahihi, hasa kwa wale ambao si mahiri katika Kiswahili. Watu hao, kwa maoni ya Massamba (keshatajwa), huchukulia kuwa kila neno na muundo wa sentensi uliomo katika vyombo vya habari huwa ni fasaha. Kwa maelezo haya kwamba, kwa sababu ya nguvu ya vyombo vya habari kwa hadhira, upo uwezekano mkubwa wa wazungumzaji wa Kiswahili kupotoshwa juu ya matumizi ya maneno na hivyo kuzungumza Kiswahili ambacho si sanifu wala fasaha.

Kwa upande wa hadhira inayomudu vyema lugha ya Kiswahili, haivumilii makosa ya msamiati kuendelea kufanyika. Kwanza, hadhira inaweza kupuuza habari za vyombo husika kwa sababu ya kukerwa na makosa. Pelg (keshatajwa) ameandika kuwa habari ambayo ina makosa ya lugha hukera hadhira hasa makosa yanapozidi. Pili, hadhira huamua kukosoa makosa hayo kwa kuwa ina uelewa wa masuala ya lugha. Tatu, hadhira huviandikia vyombo vya habari juu ya makosa hayo na kuvitaka vibadilike na vitumie lugha sanifu na fasaha (Shoo, keshatajwa).

Athari nyingine ya makosa ya msamiati yanayofanywa kwenye vyombo vya habari ni hadhira kupata ujumbe uliopotoka. Kama alivyoandika Shoo (keshatajwa), vyombo vya habari vya *BBC Swahili* na *DW Kiswahili* vimesababisha kubadili maana ya neno *mhanga* kutokana na kulitumia visivyo sahihi. Hadhira ya matini tulizochunguza inaweza kupata ujumbe usiokusudiwa kwa sababu ya kutumia baadhi ya maneno yasiyo sahihi au kukosea kuyaandika.

Kwa mfano, tumeona kuwa maneno *salia* na *watupu* katika: a) *salia nyumbani* na b) *wanawake watupu* yalitumika vibaya katika makala zilizochunguzwa. Kutokana na uteuzi wa maneno haya, msomaji wa makala anashindwa kung'amua maana sahihi iliyolengwa kuwasilishwa na mwandishi. Hii ni kwa sababu, atafasili kwamba: a) *raia waliambiwa wafanye ibada nyumbani kwao* au *raia waliaswa wabaki/wasitoke makwao*. Katika mfano b) msomaji atafasili kwamba *wanawake walikuwa uchi* au *walikuwa ni watu wa jinsia ya kike tu*. Kwa msikilizaji ambaye hazingatii muktadha wa habari au ambaye anajifunza lugha ya Kiswahili, akisoma kauli hizo mbili (zilizotolewa mfano), anaweza kuchukulia kuwa mwandishi alimaanisha 'raia kufanyia ibada nyumbani mwao' na 'wanawake walikuwa uchi', hivyo kupata ujumbe uliopotoshwa.

Kwa upande wa lugha ya Kiswahili, makosa ya msamiati huharibu usanifu na ufasaha wa lugha. Badala ya kutumia lugha fasaha kwa kuteua maneno sanifu, vyombo vya habari (BBC na DW) hutumia misamiati isiyo sanifu, iliyokosewa au iliyotumika kimakosa. Jambo hili huharibu usanifu na ufasaha wa lugha kwani watumiaji wa Kiswahili ambao si mahiri na wanafuatilia matangazo ya vyombo hivi, huyatumia maneno yaliyokosewa wakiamini kwamba ni sahihi kwa kuwa yametumika katika vyombo vya habari. Matokeo ya hali hii ni kuwa na lugha ya Kiswahili iliyosheheni makosa mbalimbali ya msamiati. Kulingana na Idarus (2010), watumiaji wa lugha ya Kiswahili hufanya makosa yanayoharibu ufasaha na usanifu wa Kiswahili. Miongoni mwa makosa hayo ni ya kimsamiati ambapo wazungumzaji huteua msamiati usiostahili katika matumizi yao. Pia, wazungumzaji wa Kiswahili huchanganya maana za baadhi ya misamiati wanayoitumia, na hivyo kupotosha maana na matumizi sahihi ya maneno hayo (Idarus, keshatajwa). Hali hii husababishwa na matumizi mabaya ya maneno katika vyombo vya habari kutokana na watumiaji wa Kiswahili kusikiliza au kusoma lugha yenye makosa ya msamiati. Lakini, jambo jema ni kwamba, kwa baadhi ya wasikilizaji walio mahiri wa lugha, hali ya kubananga Kiswahili huwa haivumiliki (Shoo, keshatajwa). Katika jamii kama Sirilanka, baadhi ya hadhira ya vyombo vya habari hupinga matumizi yanayoweza kuharibu lugha yao (Ranasuriya, 2015).

Kwa sasa, Kiswahili kinakabiliwa na changamoto ya matumizi ya lugha yasiyo sahihi kama matumizi mabaya ya maneno, kubanangwa kwa sarufi na miundo isiyo sahihi ya Kiswahili

katika vyombo vya habari (King’ei, 2002; Sigalla, 2019). Kiango (2002) ameandika kwamba faida kubwa ya sera ya matumizi ya Kiswahili katika vyombo vya habari ni kusaidia kusambaza Kiswahili kwa haraka na kukuza uwezo wa lugha wa watumiaji wake. Faida ya pili ni kwamba vyombo vya habari vitasaidia katika kufikisha habari kwa watu wengi ambao kwa namna moja au nyingine hawajui Kiingereza (na lugha nyingine za kigeni). Kutokana na maelezo ya Kiango (keshatajwa), mchango wa vyombo vya habari katika Kiswahili ni kukitumia kwenye matangazo yake pia kukisambaza kwa watu wengi kupitia habari. Swali la kujiuliza ni: *Je, ni Kiswahili cha namna gani vyombo hivi vinatumia na kukisambaza kwa wasilikizaji wake?* Kama vyombo hivi vitatumia Kiswahili sanifu na fasaha, basi hadhira itafaidi; na hivyo, kuimarisha Kiswahili. Endapo Kiswahili kinachotumiwa kimejaa kila aina ya makosa, basi lugha ya Kiswahili itakuwa imepotoshwa na kuharibiwa.

Mapendekezo

Kutokana na matokeo ya utafiti huu, tunapendekeza mambo yafuatayo:

- a) Waandishi wa habari wanapaswa kujenga tabia ya kusoma maandiko mbalimbali yanayohusu stadi ya uandishi; pia, wajifunze kila mara matumizi ya msamiati kwa kutumia kamusi na vitabu vya istilahi za fani mbalimbali za Kiswahili (Sigalla, keshatajwa). Usomaji huo utawasaidia kujua matamshi, maandishi na maana za maneno ya lugha ya Kiswahili.
- b) Mamlaka za vyombo husika vya habari zitoe fursa kwa wanahabari kuhudhuria mafunzo na semina mbalimbali zinazohusu matumizi ya lugha fasaha na sanifu. Jambo hili litawasaidia wanahabari kujua matumizi sahihi ya msamiati wa Kiswahili katika mazungumzo na maandishi.
- c) Wanahabari watie mkazo katika kufanya uhariri wa kina na makini kabla ya habari kuchapishwa ili kutambua na kusahihisha makosa ya kiuandishi.
- d) Somo la lugha hasa Kiswahili linapaswa kuwa sehemu ya masomo ya taaluma ya habari na mawasiliano. Wanahabari wanaofaulu vizuri somo hili wapewe kipaumbele katika kuajiriwa. Hii itawasaidia wanahabari kuepuka kufanya makosa ya mara kwa mara katika kuripoti habari.

Hitimisho

Makala hii imechunguza makosa ya msamiati wa Kiswahili katika *BBC Swahili* na *DW Kiswahili* kwa kumakinikia matini andishi tu. Zaidi, makala imejadili athari za makosa hayo kwa hadhira ya vyombo vya habari vya Kiswahili kwa ujumla. Japo makala hii imeshughulikia makosa yanayohusu msamiati tu, bado unahitajika utafiti wa kina wa makosa mengine katika *BBC Swahili* na *DW Kiswahili* kama makosa ya uakifishaji na matumizi ya lugha. Kwa hiyo, uchunguzi wa matumizi ya Kiswahili katika vyombo vya habari vya kimataifa na ndani ni muhimu kwa ukuzaji wa lugha ya Kiswahili. Azma ya Waswahili kukifanya Kiswahili kuwa lugha ya dunia itatimia ikiwa wadau wataendelea kufanya uchunguzi unaolenga kurakibisha makosa na kuimarisha matumizi bora ya Kiswahili katika vyombo vya habari.

Marejeleo

- Akbari, E. & Kheirabadi, R. (2015). A Linguistic Analysis of Errors in News Agencies and Websites of Iran. *Theory and Practice in Language Studies*, 5, 11: 2340- 2347.
- Alqahtani, M. (2015). The Importance of Vocabulary in Language Learning and How to Be Taught. *International Journal of Teaching and Education III*, 3: 21-34.
- Aruba, B. K. (2017). *Makosa ya Kisemantiki katika Mawasiliano Andishi ya Kiswahili Miongoni mwa Wanafunzi wa Shule za Upili: Mfano wa Kaunti ya Kakamega*. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Maasai Mara.
- BAKITA. (2015). *Kamusi Kuu ya Kiswahili*. Toleo la 1. Longhorn Publishers.
- Gbara, N. B. (2001). *Grammatical Errors in the Nigerian Print Media and their Effect on Audience Perception and Behaviour*. Tasnifu wa Uzamili haijchapishwa, University of Nigeria.
- Idarus, A. S. (2010). Makosa Yanayofanywa Mara kwa Mara katika Matumizi ya Kiswahili. Katika TUKI (Wah.), *Makala za Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili 1: Lugha ya Kiswahili* (Tol. 3, uk. 173-187.), TUKI.
- Jurianto, R. A. (2015). An Analysis of Lexical Errors in the English Narrative Writing Produced By the Tenth Grade Students of SMA Negeri 9 Surabaya in EFL Classroom. *Anglicist*, 04, 02: 69-79.
- Kemunto, A. B. & Ontieri, J. O. (2018). Vyanzo vya Makosa ya Kisemantiki katika Mawasiliano Andishi ya Wanafunzi wa Shule za Sekondari nchini Kenya. Katika M. Mukuthuria na M. Kandagor (Wah.), *Lugha ya Kiswahili: Utafiti na Maendeleo yake* (uk. 168-173). TATAKI.
- Kiango, J. G. (2002). Nafasi Ya Kiswahili Katika Ujenzi wa Jamii Mpya ya Afrika Mashariki. *Nordic Journal of African Studies* 11(2):185-197.
- Kihore, Y. M. (2004). Masuala ya Kisarufi katika Magazeti ya Mitaani ya Kiswahili – Tanzania. *Swahili Forum XI*: 107-119.

- King'ei, K. (2000). Matatizo ya Matumizi ya Lugha katika Vyombo vya Habari: Mifano kutoka Kenya. (AAP) 64: *Swahili Forum* VII: 45-56.
- Kitsao, R. S. (2015). *Uchanganuzi wa Makosa ya Kisarufi katika Insha za Wanafunzi wa Shule za Msingi na Yavyochangia Matokeo Mabaya ya Mitihani, Kata ya Ganze, Kaunti ya Kilifi, Kenya*. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Pwani.
- Kordjazi, Z. (2011). The Effect of Word Frequency on Answering Grammar Questions. *Journal of Language Teaching and Research* 2, 6: 1425-1429.
- Massamba, D. P. B. (1995). Kiswahili kama Lugha ya Mawasiliano. Katika Mlacha, S.A.K.(Mh.), *Kiswahili katika Kanda ya Afrika Mashariki: Historia, Matumizi na Sera* (uk.1-11). TUKI.
- Onyango, J. O. & Odawo, M. A. (2016). Kiswahili kama Chombo cha Kutangaza na Kuuza Vyombo vya Habari nchini Kenya. *Mulika* 35: 87-97.
- Ontieri, J. O. (2015). Athari za Kifonolojia za Lugha ya Kwanza katika Kiswahili: Mfano wa Lugha Teule za Kibantu Nchini Kenya. *Mulika* 34: 1-13.
- Ranasuriya, D. (2015). Effects of Radio and Television Media on Language. *Journal of Mass CommunicatJournalism* 5, 6: 265-271.
- Shoo, G. (2004). Nafasi ya Kiswahili katika Vyombo vya Habari Wakati Huu wa Utandawazi. Katika BAKITA (wah.), *Kiswahili na Utandawazi* (uk.79-87). BAKITA.
- Sigalla, O. (2019, 12 Julai). Vyanzo vya Upotoshaji Lugha katika Uandishi. *Habarileo Ijumaa*, uk.11.
- Simba, J.A. (1995). Umuhimu wa Kuwa na Sera katika Idhaa za Kiswahili. Katika Mlacha, S.A.K. (Mh), *Kiswahili katika Kanda ya Afrika Mashariki: Historia, Matumizi na sera* (uk.58-65). TUKI.
- Tanyer, S. & Ozturk, Y. (2014). Pre-Service English Teachers' Vocabulary Learning Strategy Use and Vocabulary Size: A Crosssectional Evaluation. *Journal of Language Teaching and Research* 5, 1: 37-45.
- TATAKI. (2013). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Tol. 3. Oxford University Press.

- Telg, Ricky. (2015). News Writing for Television and Radio. *Department of Agricultural Education and Communication, UF/IFAS Extension*. <http://edis.ifas.ufl.edu>.
- Viera, R.T. (2017). Vocabulary Knowledge in the Production of Written Texts: A Case Study on EFL Language Learners. *Revista Tecnológica ESPOL – RTE* 30, 3: 89-105.
- Yang, W. (2010). A Tentative Analysis of Errors in Language Learning and Use. *Journal of Language Teaching and Research* 1, 3: 266-268.
- Zafar, A. (2016). Language Effectiveness in print media advertisements of Multi-National Fast Food chains. *The European Proceedings of Social & Behavioral Sciences*, 132 -139.